
# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS
TANZANIA

Toleo la 88
Januari - Februari 2020

## NORWAY YATOA NYONGEZA YA DOLA ZA MAREKANI MILIONI 4.3 KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA PAMOJA YA KIGOMA (KJP)




Mheshimiwa Hans Corneliussen, Mshauri wa Mambo ya Siasa katika Ubalozi wa Norway (kushoto), akikabidhi hundi ya dola milioni 4.3 kwa Mheshimiwa Michael Dunford, Mratibu Mkazi wa UN a.i. (kulia) kusaidia utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Kigoma. (Katikati) Brigedia Jenerali Mstaafu Emmanuel Maganga, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma. **Picha | *Grace Mongi / UN Tanzania***

Mapema mwaka huu, Ubalozi wa Ufalme wa Norway ulitoa nyongeza ya Dola za Marekani Milioni 4.3 (Karibu sawa na Shilingi za Tanzania Bilioni 9.9) kwa Umoja wa Mataifa ili kusaidia utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP), na hivyo kufanya jumla ya mchango wa Norway katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAPII) (2016-2021) nchini Tanzania kufikia Shilingi Bilioni 60.

Programu ya KJP ni ya kisekta na inatekelezwa kwa pamoja na Mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na mamlaka za mkoa na wilaya kwa lengo la kuongeza kasi

*Inaendelea Ukurasa wa pili (2)*

## VIDOKEZO

- Vijana nchini Tanzania wadai ubora wa elimu, mafunzo na huduma zilizo rafiki kwao
- Kuendeleza ubunifu katika kukabili changamoto za dunia
- Kufika kila kona ... kwa baiskeli!
- Washindi wa Shindano la Bishara Rafiki kwa Mazingira kunufaika na Mradi wa ILO wa Green Jobs

## Kauli ya Serikali

***"Ningependa kuanza kwa kutoa shukrani kwa msaada mkubwa ambao Umoja wa Mataifa Tanzania imetoa katika mkoa kupitia Programu ya Pamoja ya Kigoma. Kwa mwendelezo huohuo, ningependa kuwashukuru washirika wote wa maendeleo waliochangia katika programu hii hasa Norway, Ireland na Sweden. Sisi watu wa Kigoma tunauthamini sana mchango wenu."***

**Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali Mstaafu Emmanuel Maganga wakati wa Mkutano wa 4 wa Kamati ya Uongozi ya Programu ya Pamoja ya Kigoma uliofanyika Februari 4, 2020 katika Mkoa wa Kigoma.**

*Kutoka ukurasa wa Kwanza (1)*

ya maendeleo katika jamii za Mkoa wa Kigoma ambazo hivi sasa zimewapokea wakimbizi na watafuta hifadhi 278,000.

Akizungumza wakati wa utiaji saini Mjini Kigoma, Bw. Hans Corneliussen, ambaye ni Mwambata wa Masuala ya Kisiasa katika Ubalozi wa Norway, alisisitza umuhimu wa ushirikiano wa karibu kati ya Umoja wa Mataifa na tawala za mikoa na kusisitiza kwamba ushiriki wa jamii ulikuwa muhimu ili kujenga umiliki wa programu hiyo na kuimarisha maisha ya watu wa Mkoa wa Kigoma.

Norway ni mwungaji mkono madhubuti wa Mfuko wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa (UN One Fund) na msaada wake kwa KJP unamaanisha kwamba zaidi ya wakulima wadogowadogo 9,000 wamejenga taratibu bora za uvunaji na uhifadhi mazao; Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zimeanzishwa katika halmashauri nne ambako KJP inatekelezwa; na wajasiriamali vijana na wanawake 12,894 wamenufaika na mafunzo ya kuongeza ujuzi, usimamizi wa biashara na kuwezesha upatikanaji wa fedha. Ujenzi na ukarabati wa mifumo 11 ya usambazaji maji na pia maeneo ya usafi binafsi na wa mazing ira



Picha ya pamoja ya ujumbe (Maofisa kutoka Balozi za Ireland, Ufalme wa Norway na Sweden, Serikali, na Umoja wa Mataifa) wakati wa Mkutano wa Kamati ya Uongozi ya Programu ya Pamoja ya Kigoma uliofanyika Mkoa wa Kigoma, mwezi Februari. **Picha|*Msafiri Manongi / UN Tanzania***

katika shule na jamii nao pia umeanza.

Bw. Michael Dunford, ambaye ni Kaimu Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na Mwakilishi wa Nchi wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP), na ambaye alishiriki katika tukio hilo, aliishukuru serikali ya Ufalme wa Norway na watu wake kwa kudumisha misaada kusaidia kazi za Umoja wa Mataifa. "Norway imekuwa mshirika madhubuti wa Tanzania na Umoja wa Mataifa kwa miongo mingi. Kwa kulenga mahitaji ya jamii ya watu wa mkoa huu (Kigoma), rasilimali hizi zitatuwezesha kuendeleza mafanikio yaliyokwishapatikana hadi sasa kupitia KJP, kuongeza kasi ya maendeleo kulekea katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu."

Kwa niaba ya Serikali, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Mh. Brigedia Jenerali Maganga, aliishukuru Norway na washirika wa maendeleo kwa kuwasaidia watu wa Kigoma, ambapo aliahidi ushirikiano wake ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi na tija kutokana na programu hiyo.

Mchango wa Norway utatolewa kupitia Mfuko wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa, ambao ulianzishwa kuwezesha mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini kutekeleza Mpango wa UNDAP II.


This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: https://tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

## KUFIKA KILA KONA ... KWA BAISKELI!




Baiskeli za UNFPA zitasaidia waelimisha rika katika Mkoa wa Simiyu kufanya kazi yao kwa urahisi zaidi. **Picha|*Ally Mgoo / UNFPA Tanzania***

Vikundi sita vya Waelimisha rika kutoka katika mpango unaosimamiwa na UNFPA wa Vikundi Rafiki kwa Waliobalehe na Vijana (Adolescent and Youth-Friendly (AYF) Corners) katika Mkoa wa Simiyu kila mmoja amekabidhiwa baiskeli ili kurahisisha kazi yao ngumu wanayofanya katika jamii.

Hivi sasa jumla ya waelimisha rika 30 wamekabidhiwa baiskeli zilizotolewa na UNFPA kwa fedha kutoka katika Shirika la Korea la Ushirikiano wa Kimataifa (KOICA) kama sehemu ya Mradi wa Nilinde Nikulinde kwa lengo la kuwasaidia kufika mbali zaidi wanaposafiri katika maeneo yao na mengineyo ili kuhamasisha mabadiliko ya tabia kupitia utoaji elimu kuhusu afya ya ngono na uzazi (SRH). Baiskeli nyingine 35 zitagawiwa kwa vikundi saba vilivyobaki vya AYF baadaye mwezi huu mkoni Simiyu.

Waelimisha rika 65 katika Mkoa wa Simiyu ambao walifuzu mafunzo yaliyoendeshwa na washirika wa UNFPA, Kiota Women's Health and Development's (KIWOHEDE), ambapo mafunzo yalihusu afya ya ngono na uzazi na haki zake hufanya kazi pasipo kuchoka katika kutoa elimu ya kuondoa mila potofu na kuwasaidia wanarika wenzao kufanya uchaguzi sahihi na unaotokana na utafiti kuhusu masuala ya afya ya ngono na uzazi kwani masuala hayo yana taathira kubwa kwa maisha yao ya baadaye. Wao ni sehemu ya mtandao wa wanarika chini ya UNFPA nchini Tanzania ambao tayari wamewafikia zaidi ya mabarubaru na vijana 80,000 kwa kuwapa elimu ya afya ya ngono katika mwaka 2019, miongoni mwa waliofikiwa ni pamoja na vijana walio nje ya mfumo wa elimu.

Waelimisha rika pia ni viungo muhimu kwa Vijiwe 13 vya

*Inaendelea Ukurasa wa Nne (4)*

*Kutoka ukurasa wa Tatu (3)*

Waliobalehe na vijana ambavyo vimeanzishwa kwa kupewa nafasi katika vituo vya afya vilivyokarabatiwa na kupewa vifaa na UNFPA katika Mkoa wa Simiyu tangu mwaka 2018 kupitia Mradi wa miaka miwili wa Nilinde Nikulinde. Vijiwe hivyo vinatoa mazingira salama na wezeshi kwa vijana waliobalehe walio hatarini na vijana wengine ili wao kukutana na kupata huduma mbalimbali za Afya ya Ngono na Uzazi ikiwemo uzazi wa mpango, upimaji na nasaha za hiyari kwa VVU, ushauri wa kisaikolojia, na elimu kuhusu namna ya kujihudumia kwa usalama wakati wa hedhi. Waelimisha rika hutoa elimu kuhusu huduma zinazopatikana katika vijiwe hivyo na kutoa rufaa zinazohitajika.

Huku ikiwa imebaki miaka 10 ya kutekeleza Malengo ya Dunia ya Maendeleo Endelevu, UNFPA inaongeza juhudi kuhakikisha kwamba vijana nchini Tanzania, hasa wasichana walio kwenye balehe, wanapata huduma kamili za taarifa kadiri ya rika, elimu na huduma za afya ya ngono na uzazi kokote wanakoishi ili waweze kupita salama kipindi cha mpito na kuingia utu uzima kwa namna yenye tija ambapo hakuna yeyote anayepaswa kuachwa nyuma.

## JUHUDI ZA KUKOMESHA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO ZAPAMBA MOTO ZANZIBAR



Washriki wa mafunzo ya IOM wakiwa na mgeni rasmi, Bi. Wahida Maabad Mohamed, Mkurugenzi wa Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii ya Zanzibar; na Bw. Ahmed Saidi Mwen-dadi, Mkuu wa Mafunzo, Utetezi na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Mambo ya Nje ya Zanzibar. **Picha| Agnes Kenneth/ UN Tanzania**

Vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto Visiwani Zanzibar ni jambo la kawaida. Kwa mujibu wa Utafiti wa Demografia na Afya nchini Tanzania wa 2015/16, asilimia 14 ya wanawake wanafanyiwa vitendo vya ukatili Zanzibar.

Usafirishaji haramu wa binadamu, ambao ni aina ya ukatili dhidi ya wanawake na Watoto mara nyingi ni matokeo ya ukosefu wa usawa wa kijinsia na hadhi ya chini ya kijamii wanayopewa wanawake na watoto katika familia na jamii.

Shirika la Kimataifa la Wahamiaji (IOM), kupitia Programu ya Pamoja ya Zanzibar (ZJP), linashirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto Visiwani Zanzibar, na, mwezi Januari 2019, shirika liliandaa mafunzo ya siku mbili kuhusu unyanyasaji wa kibiashara, ikiwemo usafirishaji haramu wa wanawake na watoto, kwa kushirikiana na Sekretariati ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Mafunzo hayo yaliwaleta pamoja washiriki 20 kutoka katika wizara za serikali zenye dhamana na pia wawakilishi

*Inaendelea Ukurasa wa Tano (5)*

*Kutoka ukurasa wa Nne (4)*

kutoka katika Idara ya Uhamiaji, Idara ya Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama. Mafunzo yalilenga kuimarisha uratibu kati ya wenye dhamana huko Zanzibar kutafuta ufumbuzi wa tatizo la usafirishaji haramu wa wanawake na watoto kama moja ya aina ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kukuza uelewa na kuimarisha sheria kwa lengo la kuandaa mwitikio ulioratibiwa vema katika utoaji wa huduma za kinga, msaada na rufaa kwa wanawake na watoto manusura wa biashara haramu ya usafirishaji binadamu na vitendo vya ukatili.

Mgeni Rasmi, Bi. Wahida Maabad Mohammed, Mkurugenzi wa Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii, aliwaasa washiriki kuwashirikisha maarifa hayo maofisa wenzao serikalini na katika jamii ili kukomesha usafirishaji haramu wa wanawake na watoto na aina nyingine za vitendo vya ukatili. Mtandao wa watu ambao wamedhamiria kukomesha usafirishaji haramu wa binadamu na ina nyingine za ukatili Zanzibar uliundwa wakati wa mafunzo hayo.

## KUENDELEZA UBUNIFU KATIKA KUKABILI CHANGAMOTO ZA DUNIA




Kutoka Kushoto: Anna Ferracuti (UNCDF), Asia Sultan (WFP), Emmanuel Bayo (UNICEF), Peter Nyanda (UNDP), Faith Shayo (UNESCO), Victor Akim (UNIDO), na Catherine Rose Barretto wakijadili kuhusu ubunifu kiakili wakati wa Usiku wa Ubunifu kuhusu namna mashirika tofauti ya UN yanaweza kutumia teknolojia ya kisasa ili kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).
**Picha|*WFP Tanzania***

Mnamo tarehe 23 Januari, 2020, Umoja wa Mataifa Tanzania, Kitovu cha Ubunifu Tanzania cha Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Mtandao wa Ubunifu wa Umoja wa Mataifa (UNIN) ziliandaa tukio la kwanza la aina yake la Usiku wa Ubunifu wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania.

Tukio hilo lilionyesha kazi mbalimbali za ubunifu zinazoendelea na kuonyesha utayari wa Umoja wa Mataifa katika kutumia mbinu za kiubunifu ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Njia mpya za kufanya kazi na utamaduni unaowezesha ubunifu na ufanyaji majaribio ni mambo muhimu katika kuleta njia mpya za kufanya kazi katika Umoja wa Mataifa. Na ili kuwezesha mabadiliko haya ya kiutamaduni, mashirika mengi ya Umoja wa Mataifa hivi sasa yameanzisha timu maalumu kwa ajili ya kuhamasisha ubunifu katika ngazi za dunia, kanda na nchi.

Akizungumza katika tukio hilo, Bw. Michael Dunford, ambaye ni Mwakilishi wa Nchi wa WFP Tanzania, alisisitiza kwamba suala la kufanya mambo kwa mazoea halitasaidia kufikiwa kwa SDGs, na kwamba ni lazima kuweko na utayari wa kushirikiana katika kutumia teknolojia mpya na kufikiri kiubunifu ili kuufanya Umoja wa Mataifa kuwa mstari wa mbele katika

*Inaendelea Ukurasa wa Sita (6)*

*Kutoka ukurasa wa Tano (5)*

> *"kufanya mambo kwa mazoea halitasaidia kufikiwa kwa SDGs, na kwamba ni lazima kuweko na utayari wa kushirikiana katika kutumia teknolojia mpya na kufikiri kiubunifu ili kuufanya Umoja wa Mataifa kuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na baadhi ya changamoto kubwa zinazoikabili dunia leo."*
>
> **Michael Dunford, Mwakilishi Mkazi wa WFP Tanzania**

kukabiliana na baadhi ya changamoto kubwa zinazoikabili dunia leo.

Usiku wa Ubunifu ulikuwa ndio mwisho wa majuma nane ya Safari ya Ubunifu Tanzania mfululizo wa mafunzo ya muda mfupi ya ubunifu ili kubaini changamoto katika safari ya kufikia SDGs ambapo washiriki walijifunza jinsi ya kuendeleza masuluhisho yanayowezekana kwa kutumia mbinu za kiubunifu. Katika Safari hiyo, vikundi sita kutoka katika taasisi tofauti za Umoja wa Mataifa zilishirikiana kubaini changamoto mtambuka na masuluhisho ya kiubunifu ya kusaidia kuongeza kasi kuelekea katika ufikiwaji wa SDGs.

Katika Usiku wa Ubunifu, kila timu ilipewa dakika tatu za kujenga hoja ya fikra zao. Timu utoka WFP iliandaa wazo la njia ya upashanaji habari kwa kutumia simujanga na kionyesha filamu kidogo ili kutangaza maudhui ambayo yangaweza kuwafikia zaidi ya Watanzania milioni 40.




Mwakilishi Mkazi wa WFP, Bw. Michael Dunford, akihutubia hadhira wakati wa Usiku wa Ubunifu kuhusu namna ya ubunifu unaweza kuiubua njia mpya za kutekeleza kazi za UN. **Picha|*WFP Tanzania***

Safari ya Ubunifu iliandaliwa na Kitovu cha Ubunifu cha WFP, UNIN, na kusaidia na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, na ilishirikisha mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa ambapo washiriki walijifunza kuhusu zana tofauti za msingi za ubunifu na njia ambazo wangeweza kuzitumia katika maeneo yao ya utendaji kazi.

Kambi za mafunzo ya muda mfupi zinaweza kuanzishwa na kuongezwa kwa wingi ndani na nje ya Tanzania.

*Inaendelea Ukurasa wa Tatu (7)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: https://tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa Sita (6)*




Alice Maro, Ofisa wa Mawasiliano kutoka Mpango wa Chakula Duniani (WFP) akieleza jinsi chombo cha habari cha kisasa, kinachotumia simu ya mkononi na kionyesha picha (projector), ambacho kitasaida kazi ya UN ya kuwafikia wale walio hatarini zaidi kwa kuwafikishia misaada ya kibinadamu na ujumbe wa maendeleo. **Picha|*WFP Tanzania***

## VIJANA NCHINI TANZANIA WADAI UBORA WA ELIMU, MAFUNZO NA HUDUMA ZILIZO RAFIKI KWAO




Machampioni wa Ajenda ya Watoto na Vijana wakizindua Ajenda katika kilele cha Sherehe za CRC@30. **Picha|*Studio 19***

Watoto na vijana nchini Tanzania wameanzisha vuguvugu ili kuhakikisha kwamba sauti zao zinasikika katika ngazi za juu kabisa za utoaji wa maamuzi nchini. Mnamo Januari, karibu watoto 300 kutoka katika mitandao na majukwaa mbalimbali walishiriki katika Mkutano wa Vijana ulioandaliwa na Femina Hip kwa kushirikiana na UNICEF.

Mkutano huo ulikuwa ni hatua nyingine muhimu katika vuguvugu hilo ili kuhakikisha sauti za vijana na watoto zinasikika;

*Inaendelea Ukurasa wa Nane (8)*

*Kutoka ukurasa wa Saba (7)*

safari ambayo ilianza mapema mwaka 2019 kama sehemu ya kumbukumbu ya 30 ya Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC@30), ambapo, kwa msaada kutoka UNICEF, zaidi ya watoto na vijana 34,000 walikusanyika na kuandaa Ajenda ya Watoto na vijana azimio lililobeba matumaini yao kwa Tanzania ya baadaye. Shughuli za uwandani pia ziliwafikia zaidi ya watoto na vijana milioni 9 kupitia vyombo vya serikali, vyama vya kiraia, mitandao inayoongozwa na vijana na majukwaa ya mashuleni ili kutoa elimu kuhusu haki za watoto na kudai utekelezaji na uendelezaji wa haki hizo. Ajenda ya Watoto na Vijana inajenga msingi wa vijana vinara kuongoza mikutano ya utetezi kwa kukutana na wadau tofauti wakimemo watendaji wa juu wa makampuni, viongozi wa dini, wafadhili na washirika wa maendeleo na Wabunge wa Muungano na Zanzibar. Wadau wote ambao watajadili Ajenda na vijana wanaweka nia ya kuchukua hatua kuleta mabadiliko.

Katika Mkutano wa Vijana, vijana walibaini maeneo muhimu matatu kutoka katika Ajenda ambayo ni ya kipaumbele katika mwaka 2020: Kuimarishwa kwa mtalaa wa elimu na kuongeza idadi ya mabalehe wanaohitimu elimu ya sekondari; uwezeshaji kiuchumi, kwa kuweka mkazo katika kujenga fursa kwa wanaojitolea na wanafunzi walio mafunzoni ili kuwaandaa vijana kwa ajili ya soko la ajira; na upanuzi wa ufikiwaji wa huduma zilizo rafiki kwa vijana, hasa suhula au miundombinu inayoongeza upatikanaji wa taarifa na huduma za afya ya ngono na uzazi na haki zinazohusiana nazo.

Mapendekezo yamezingatia wakati ambapo nchi inaelekea katika Uchaguzi Mkuu baadaye mwaka huu.




Mwakilishi wa UNICEF Shalini Bahuguna (kushoto) akihutubia katika mkutano mkuu wa vijana uliofanyika jijini Dar es Salaam. Anayetazama ni Mkurugenzi wa Vyombo vya Habari wa Femina Hip, Amabilis Batamula. **Picha|*UNICEF Tanzania***

*Inaendelea Ukurasa wa Tisa (9)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: https://tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa Nane (8)*

Mchakato wa uandaaji Ajenda hiyo, mikutano iliyofuatia ya ushawishi kwa wenye kutoa maamuzi, na Mkutano Mkuu wa Vijana yote inawezesha kuleta ushiriki wenye maana wa vijana katika mchakato wa kutoa maamuzi, ambalo ndiyo kiini cha kazi ya Generation Unlimited nchini Tanzania. Hivi sasa watoto na vijana sasa wanataka muundo-dhana mpya ambao utawachukulia watoto kama wadau zaidi kuliko wanufaika, ya sheria na dola, lakini kama wadau, ambao wanajua nini wanataka kwa maana ya sera, vipaumbele na majukwaa ya utoaji huduma jambo ambalo linaziweka sauti na mawazo yao katika mstari wa mbele wa maendeleo endelevu nchini Tanzania.



Watoto wakijadili katika moja ya mikutano ya mashauriano huko Mbeya. **Picha | *UNICEF Tanzania***

## WADI MPYA YA AKINA MAMA ITAIMARISHA UBORA WA MATUNZO NA MATOKEO YA AFYA KWA WANAWAKE WA WILAYA YA KASULU, MKOA WA KIGOMA

Mwezi uliopita, Maria alilazimika kusafiri umbali wa maili 25 ili kujifungua mtoto wake katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu. Mama huyo alikuwa akisumbuliwa na kifafa cha mimba ambacho kilikuwa karibu kimwue na hata mtoto wake wa kiume alikuwa hatarini. Hata hivyo, rafiki yake Maria, ambaye hivi sasa ni mjamzito wa mimba yake ya kwanza sasa hatalazimika kuondoka nyumbani kwake kabla ya kujifunga yeye atapata huduma kutoka kwa mkunga mwenye mafunzo wakati wa kujifungua katika wadi ya akina mama wazazi iliyojengwa hivi karibuni katika Zahanati ya Muzye.

Wadi hiyo ya wazazi katika Zahanati ya Muzye katika Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma iliyofunguliwa na Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Simon Anange, mnamo Februari 3 hivi sasa ina vyumba vitatu tofauti, chumba cha manesi, bafu, na mfumo wa maji ulioimarishwa, na itawekewa vifaa vyote ili kutoa huduma bora mbalimbali za afya ya uzazi, akina mama, watoto wachanga na watoto (RMNCH).

Ukarabati huo ni sehemu ya msaada unaotolewa na UNFPA kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuzuia vifo ya akina mama na watoto wachanga kwa kuongeza matunzo ya wakati na yenye kuzingatia ujuzi wakati wa ujauzito na kujifungua, ikiwemo matunzo ya wakati za dharura pale kunapokuwa na matatizo ya uzazi. Sasa wanawake 21, ambao ni wastani ya wanawake wanajifungua kwa mwezi katika eneo linalohudumiwa na zahanati hiyo, wataweza kuwa mama kwa usalama zaidi, jambo linaloongeza kasi ya Tanzania katika kutimiza ahadi zake za kitaifa na katika ngazi ya dunia.

*Inaendelea Ukurasa wa Kumi (10)*

*Kutoka ukurasa wa Tisa (9)*

Kazi ya UNFPA ya kuongeza ubora wa vituo vya afya na kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya katika wilaya nne za Mkoa wa Kigoma kama sehemu ya shughuli zinazotekelezwa chini ya mradi wa Ujana Wangu -Nguvu Yangu unaofadhiliwa na Serikali ya Ireland. Zahanati ya Muzye ilikuwa miongoni mwa vituo tisa vilivyobainishwa ili kufanyiwa ukarabati na kwa ushirikiano kati ya UNFPA, tawala za mikoa na serikali za mitaa mwaka 2018. Ndani ya mwaka jana, wadi sita za akina mama zilijengwa na tatu kati ya hizo ziko katika hatua ya mwisho ili kukamilika. Vituo vyote vya afya vilivyokarabatiwa vimewekewa vifaa bora kwa ajili ya huduma kabla na wakati wa kujifunga, na hata baada ya kujifungua. Katika mwaka wa pili wa Mradi wa Ujana, vituo 12 vya afya vitakarabatiwa.

UNFPA vilevile inategemea uwekezaji katika miundombinu na vifaa kwa kusaidia utoaji mafunzo kwa watumishi katika vituo vya afya vilivyokarabatiwa ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma bora kwa akina mama waliojifungua, watoto wachanga na watoto, zikiwemo zile za dharura ya uzazi pingamizi na matunzo ya watoto wachanga. Na kampeni itazinduliwa katika eneo ambako kituo cha afya kinahudumia ili kukuza uelewa na matumizi ya huduma zinazotolewa.

UNFPA inaendelea kuunga mkono juhudi za kuongeza kasi katika kuzuia kabisa vifo vya akina mama wakati wa kujifungua hapo ifikapo mwaka 2030, kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote anayeachwa nyuma katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya dunia nchini Tanzania.



Wanawake wajawazito sasa wanaweza kupata huduma za matunzo kwa haraka na kutoka kwa watumishi wenye ujuzi. Huduma hizi ni pamoja na matunzo wakati wa ujauzito, kujifungua, na katika majuma yanayofuatia baada ya uzazi. Yote haya yanafanyika katika wadi ya wazazi ya Zahanati ya Muzye baada ya ukarabati. **Picha|Grace Mongi/*UN Tanzania***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: https://tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

# WASHINDI WA SHINDANO LA BISHARA RAFIKI KWA MAZINGIRA KUNUFAIKA NA MRADI WA ILO WA GREEN JOBS



Mmoja wa washindi, Bw. Ritchie Raphael kutoka Mkoa wa Morogoro, akipokea cheti chake kutoka kwa Prof Mhandisi Esnati Osinde Chaggu, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Katikati ni Mh. Anders Sjöberg, Balozi wa Sweden nchini Tanzania. **Picha|*ILO Tanzania***

Kama sehemu ya Mradi wa ILO wa Green Jobs nchini Tanzania, unaotekelezwa kupitia makubaliano ya ushirikiano wa dunia na Serikali ya Sweden, mashindano ya Green Challenge yaliandaliwa mwezi Desemba 2019, kwa kushirikiana na Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP) na Chama cha Warejeshelezaji cha Tanzania (TARA).

Mashindano hayo yaliwapa vijana changamoto, hasa wanawake vijana, kutuma maandiko ya ubunifu katika utunzaji wa mazingira ambayo yatasukuma mbele uanzishwaji wa biashara endelevu nchini Tanzania na kuufanya uchumi kuwa wa kijani zaidi.

Mashindano hayo yalitekelezwa kwa ushirika na watoa Huduma ya Uendeleaji Biashara Mahalia (BDS) ambao walitoa huduma zisizo za kutoza fedha katika kuleta ubunifu wa kijani na Makampuni ya Ngazi ya Kati (SMEs) yanayolenga ukuaji ili kuyasaidia kupanua biashara zao.

Kampuni zilizoingia kwenye mashindano hayo pia zilipewa fursa ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma rafiki kwa mazingira kwa kuunganishwa na programu ya ukuzaji biashara iliyofumwa pamoja, na hii ni kwa kutegemea kifurushi cha ILO kinachotambuliwa kimataifa cha Anzisha na Kuza Biashara Yako (Start and Improve Your Business (SIYB)). Kifurushi hii kinajumuisha programu ya usimamizi wa mafunnzo yanayolenga katika usimamizi bora wa biashara ndogondogo ili kutengeneza kazi zaidi na zilizo bora katika nchi zinazoendelea na uchumi ulio katika kipindi cha mpito.

Washiriki katika mashindano ya Changamoto ya Kijani walituma maandiko yao ya biashara kwa njia ya mtandao ambapo kulikuwa na maandiko 88 kutoka katika mikoa 11 ya Tanzania ambapo yalifanyiwa tathmini kwa kutumia vigezo vilivyoandaliwa kitaalamu. Washindi nane wa juu walichaguliwa kutoka katika maeneo manne tofauti Biashara ya Kijani (viwanda na huduma), Biashara za Kijani katika Kilimo, Nishati Mbadala na Usimamizi wa Takataka na Urejeshelezaji Bidhaa katika Soko.

Mh. Anders Sjöberg, Balozi wa Sweden nchini Tanzania na Prof Esnati Osinde Chaggu, Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, waliwatangaza washindi mnamo Desemba 12, 2019. Washindi, ambao ni vijana wenye mawazo ya biashara na bidhaa zilizo rafiki kwa mazingira, watashiriki katika programu ya mafunzo ya BDS ya miezi minne.

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na mbili (12)*

*Kutoka ukurasa wa Kumi na Moja (11)*

Shirika la Kimataifa la Kazi la Umoja wa Mataifa, kwa makubaliano ya ushirikiano wa jumla na Serikali ya Sweden, inatekeleza mradi wa miezi 14 wa Green Jobs ili kuhamasisha utengenezaji wa ajira zilizo rafiki kwa mazingira kwa ajili ya vijana na wanawake. Mradi huo utatumika kama kiungo muhimu katika programu kubwa zaidi za siku za baadaye.

Kwa taarifa zaidi kuhusu Mashindano ya Changamoto na washindi, tafadhali tembelea: https://youtu.be/8lBSSRtIxxQ




Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Mh. Anders Sjöberg, aliwapongeza washiriki na kuangazia kwamba ilikuwa muhimu kwa Tanzania kuwa na wajasiriamali na kampuni chomozi ambazo zinahamasisha uchumi unaojali mazingira. **Picha|*ILO Tanzania***




Washindi nane wa katika Shindano la Green Challenge walichaguliwa kutoka katika makundi manne tofauti – Kampuni za Kijani (uzalishaji viwandani au huduma), Makampuni ya Kijani ya Kilimo, Nishati Mbadala na Usimamizi wa Taka na Kurejelesha. **Picha|*ILO Tanzania***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: https://tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

# WANAFUNZI WAASWA KUJENGA DUNIA YENYE AMANI



Mh. Regine Hess, Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, akijibu maswali kutoka kwa wanafunzi kuhusu hatua ambazo Ujerumani ilizichukua mara baada ya mauaji ya halaiki ili kuhakikisha kuwa hayajirudii tena.
**Picha | Hilda Phoya/UNIC**

Mwezi Machi, zaidi ya wanafunzi 200 kutoka katika shule za jijini Dar es Salaam walishiriki katika kipindi maalumu cha kujifunza kuhusu ubaguzi dhidi ya Wayahudi na umuhimu wa kuishi pamoja katika amani kama sehemu ya kumbukubu ya Siku ya Kimataifa ya Kukumbuka Mauaji ya Wayahudi.

Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regina Hess, kwa kushirikiana na waandaaji kutoka katika Kituo cha Taarifa na Elimu cha Umoja wa Mataifa aliwahutubia wanafunzi jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Balozi aliwaelimisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa kuishi pamoja kwa amani na kusaidiana, alisisitiza kwamba: "Hakuna sababu ya kumbagua mtu yeyote miongoni mwetu." Aliongeza kwamba, "vitendo vya uhalifu dhidi ya binadamu hutendwa kila siku, ni jambo gumu sana katika baadhi ya nchi, lakini kama unaelewa kuwa vitendo hivi vinatokea kila siku kati yetu, ni rahisi kujua namna ya kupokea na kukomesha ubaguzi."

Wanafunzi hao pia walijifunza kuhusu ujumbe wa "Yasirudiwe Tena Kamwe" kutoka katika Kituo cha Taarifa na Elimu cha Umoja wa Mataifa ambapo Stella Vuzo alizungumzia mauaji ya Wahayudi milioni sita wanaume, wanawake, watoto na watu waliochukuliwa kuwa hawastahili kuishi kwa sababu ya ulemavu, imani na mwonekano wao. Alisema pia kuwa mauaji hayo yalifanywa na utawala wa Kinazi ulioongozwa na Adolf Hitler.

Ujumbe kutoka kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ulizungumzia wasiwasi unaozidi kuongezeka kuhusu "Kuibuka upya kwa chuki katika miaka ya hivi karibuni, kuanzia katika mashambulizi ya kiitikadi kali hadi yale yanayofanywa katika nyumba za ibada, jambo linaloashiria kwamba ubaguzi dhidi ya Wayahudi, aina nyingine ya ubaguzi wa kidini, ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya wengine bado ni mambo yanayotokea miongoni mwetu."

Mh. Antonio Guterres aliwataka watu wote kupiga vita chuki kwa sababu baada ya kupita miaka sabini na tano, Unazi mamboleo na ubaguzi unaofanywa na baadhi ya watu weupe, ni mambo yanayoibuka upya, na kuna juhudi zinafanywa makusudi kufifisha kumbukumbu za Mauaji ya Wayahudi na kukana kuwa yaliwahi kutokea au hata kuwaondolea hatia wauaji.

Wanafunzi walitembelea maonyesho katika Little Theatre (Ukumbi Mdogo) ambamo walitazama filamu iliyoitwa:

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na Nne (14)*

*Kutoka ukurasa wa Kumi na Tatu (13)*

"Masimulizi ya Kambi ya Auschwitz" kuhusu kesi ya siku za karibuni dhidi ya mmoja wa Wanazi, ambapo ilifanyika miaka mingi tangu Mauaji ya Wayahudi yatokee.

Programu ya elimu ya Mauaji ya Wayahudi inayoendeshwa na Umoja wa Mataifa ilianza mwaka 2005.

*"Kuibuka upya kwa chuki katika miaka ya hivi karibuni, kuanzia katika mashambulizi ya kiitikadi kali hadi yale yanayofanywa katika nyumba za ibada, jambo linaloashiria kwamba ubaguzi dhidi ya Wayahudi, aina nyingine ya ubaguzi wa kidini, ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya wengine bado ni mambo yanayotokea miongoni mwetu."*

**Regina Hess, Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania**

## SIKU ZIJAZO ZA KIMATAIFA:

**Machi 21-** Siku ya Kimataifa ya Misitu

**Machi 22 –** Siku ya Kimataifa ya Maji

**Machi 24 –** Siku ya Kimataifa ya Kifua Kikuu

**Aprili 7 –** Siku ya Kimtaifa ya Kutafakari Mauaji ya Kimbari ya Watutsi huko Rwanda.

**Aprili 7 –** Siku ya Afya Duniani

**Aprili 25 –** Siku ya Malaria Duniani

**Aprili 28 –** Siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi

## UMOJA WA MATAIFA MADHUBUTI KWA DUNIA BORA ZAIDI

**UNITED NATIONS**
TANZANIA

**Ofisi ya Mratibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa**

+255 22 219 5021

info.untz@one.un.org

Website: tanzania.un.org



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: https://tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021